

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERAKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA.

SHULE YA SEKONDARI EUGA,  
S.L.P 81,  
MAHENGE/ULANGA.

KWA MZAZI/MLEZI WA.....

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2021 KATIKA  
SHULE YA SEKONDARI EUGA.**

Rejea kichwa cha habari hapo juu.  
Ndugu mzazi/mlezi napenda kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari EUGA iliopo kata ya Euga kijiji cha Euga wilaya ya Ulanga. Shule itafunguiwa tarehe .....Mwanao asiporipoti hadi tarehe.....hatua kali zitachukuliwa dhidi wewe mzazi/mlezi. Mwanao afikapo shuleni anapaswa kuwa na mahitaji yafuatayo:

**A. SARE**

Wasichana:

- Sketi ya kaki mtindo wa rinda box ndefu (mbili)
- Shati jeupe mikono mifupi (mawili)
- Nusu kanzu na Hijabu nyeupe kwa waislamu (mbili)
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba
- Soksi nyeupe peya zaidi ya moja.
- Truck suit kwa ajili ya michezo.

Wavulana:

- suruaili ya kaki mbili yenye marinda mawili (celebrations).
- Shati jeupe mikono mifupi (mawili).
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba
- Soksi nyeusi peya zaidi ya moja.
- Mkanda wa ngozi mweusi.
- Truck suit kwa ajili ya michezo.

**B. VIFAA VYA KUJIFUNZIA DARASANI:**

- Daftali 9 kubwa
- Kalamu za wino za kutosha
- Dictionary na vitabu vya kujifunzia kingereza (muhimu sana).

**NB;**

Mwanao afahamu kuwa kingereza ndio lugha pekee ya mawasiliano inayotumika shuleni hivyo anapaswa kujifunza kingereza kwa kumpatia mahitaji muhimu yote kutoka kwako kama mzazi/mlezi kwa maslahi ya taifa na dunia.

**C. VIFAA VYA USAFI**

- o ufagio wa chelewa.
- o Kuwa na jembe na kwanja nyumbani atakuja navyo shuleni pale itakapohitajika na atarudi navyo nyumbani.

**MUHIMU:**

Mwanao anaswa kuonesha nidhamu ya hali ya juu kwa walimu, wanafunzi wenzake, wageni na watu wote wanaofika shuleni kama moto wa shule ni "ELIMIKA UTUMIKE" Mwanao anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vya darasani, michezo na elimu ya kujitegemea ili kupata ujuzi mbalimbali utakao msaidia mara baada ya kuhimu elimu ya sekondari.

Vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu havitavumilika na kupelekea hata kufukuzwa shule, hivyo wewe kama mzazi/mlezi unapaswa kumsisitiza mwanao aishi kwa kufuata sheria zote.

Uongozi wa shule ya sekondari EUGA unampongeza kupata nafasi hii adimu na unamkaribisha mwanao sana ajisikie yupo salama.

Bzulo  
MKUU WA SHULE  
SHULE YA SEKONDARI EU:SP  
S.L.P 81  
WAHANGEI/ULANGA